

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**



**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MPANGO WA UTAMBUZI NA URASIMISHAJI UJUZI**

**Je wewe ni fundi lakini ulipata ujuzi bila kupitia chuoni na kupata cheti?**

**Je una uzoefu kwenye fani yako usiopungua miaka mitano na umri wako hauzidi miaka 45?**

**Je ungependa ujuzi wako utambuliwe na kurasimishwa ili upewe cheti kulingana na ujuzi wako?**

**Kama ndivyo: Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikianana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi-VETA wanaendesha mpango wa Kutathmini na Kurasimisha Ujuzi Uliopatikana Nje ya Mfumo Rasmi wa Mafunzo. Katika mpango huu una fursa ya kufanyiwa tathmini ya ujuzi wako, kupewa mafunzo kuziba mapungufu, kisha kutunukiwa cheti. Fani zitakazohusika ni: UASHI, USEREMALA, UFUNDI MAGARI-MAKENIKA, UPISHI, UHUDUMU WA HOTELI, BAR NA MIGAHAWA.**

**Ikiwa unakidhi masharti yaliyotajwa, fika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Mji au Wilaya iliyoko karibu uchukue na kujaza fomu za maombi bila malipo. Maombi yawasilishwe kuanzia tarehe 05 hadi 25 Januari, 2017. Watakaokidhi sifa, vigezo na masharti watajulishwa kwa ajili ya usaili kuanzia tarehe 10 Februari 2017.**

**Mchakato wote wa tathmini na urasimishaji wa ujuzi utagharamiwa na Serikali. Kwa taarifa na ufafanuzi zaidi, wasiliana na Mratibu wa Programu (VETA) hii kwa namba 0715 55 55 85.**

**IMETOLEWA NA:  
KATIBU MKUU**